# GRADE 8 MID TERM 2 MAY 2022

# KISWAHILI

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako**

***Andika insha ya kusisimua itakayoanza kwa maneno haya. Ifanye iwe ya kusisimua zaidi.***

*Watoto wadogo hawafai kuajiriwa popote wala kunyanyaswa. Hii ni kwa kuwa* ..................................................................................................................................

# TARGETER WINGS DARASA LA NANE - MWAKA 2022

# MTIHANI WA MJARABU

# KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA

Wings 002

*MUDA: Saa1 dakika 40*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Umleavyo mwana, ndivyo akuavyo. Anapolelewa vyema huwa mwema akilelewa ovyo, huwa ovyo siku za usoni. Watoto wengi wana tabia __1__. Kukithiri kwa tabia mbaya __2__ vijana ni dhihirisho kuwa wazazi wameshindwa __3__ majukumu yao. Mwana wa kisasa ameachwa huru huna kutenda __4__. Iweje mwana kujibizana na mzazi __5__ ya wapita njia? Aibu iliyoje! Hatukatai watoto sharti kama ibada wapewe uhuru wa aina fulani __6__ sio wawapande wazazi wao vichwani __7__! Tangu lini __8__? Wahenga waligonga ndipo waliposema ukimcha mwana kulia utalia wewe. __9__ basi wazazi. Tuwalee wana inavyostahili na kustahiki.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** akhayari | **B.** bora | **C.** potovu | **D.** potevu |
| **2.** | **A.** miongoni mwa | **B.** pamoja na | **C.** minghairi ya | **D.** ghairi ya |
| **3.** | **A.** kutelekeza | **B.** kutekeleza | **C.** kufanyiza | **D.** kutueleza |
| **4.** | **A.** ayatakazo | **B.** alitakalo | **C.** aitakavyo | **D.** aitakayo |
| **5.** | **A.** mafichoni | **B.** pembeni | **C.** kadamnazi | **D.** mkabala |
| **6.** | **A.** lakini | **B.** ili | **C.** wala | **D.** vile |
| **7.** | **A.** kwao | **B.** mwao | **C.** vyao | **D.** pao |
| **8.** | **A.** sikio likapita kichwa | | **B.** mwenye puka akalatamu | |
| | **C.** mnyonge akapata | | **D.** mwacha mila | |
| **9.** | **A.** Abadan | **B.** Shime | **C.** Habedan | **D.** Haidhuru |

Watu wale __10__ walipoona tukiwa wajinga kama __11__. Tulikuwa tukilalamika __12__ kwa gari letu na vijana wakora waliovalia kama askari polisi. Mbona tukadanganyika __13__ jinsi hiyo? Muda si muda, mmoja wa wale wezi akapita pale akitembea asteaste. Nilipiga kite kwa hofu. Mwizi!! akakamatwa na kupigwa __14__. Alilia lakini kilio si dawa. Hatimaye akachomwa. __15__ harufu ya nguo zikichomeka. Rafiki yangu aliyekuwa akiona njaa alitapika na kuzimia zii!

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | **A.** walicheka | **B.** walitucheka | **C.** walituchekea | **D.** walituchekelea |
| **11.** | **A.** kalulu | **B.** samaki | **C.** ng'ombe | **D.** fisi |
| **12.** | **A.** kuiba | **B.** kuibiwa | **C.** kuibwa | **D.** kuibia |
| **13.** | **A.** rahisi | **B.** kirahisi | **C.** kiurahisi | **D.** virahisi |
| **14.** | **A.** kituta | **B.** kitoto | **C.** kitule | **D.** kitutu |
| **15.** | **A.** Tuliona | **B.** Tulisikia | **C.** Tulihisi | **D.** Tulinusa |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua kielezi cha wakati katika sentensi ifuatayo:
Nimekutembelea hospitalini huku mara kadhaa.
A. Nimekutembelea B. Hospitalini
C. Huku D. Mara kadhaa.

**17.** Ni pambo lipi ambalo huvaliwa kwenye uti wa pua?
A. Kishaufu. B. Herini.
C. Kidani. D. Kipuli.

**18.** Chagua nomino ya makundi iliyokosewa.
A. Umayamaya wa watu.
B. Korija la miti.
C. Kitopa cha viti.
D. Ufefe wa mahindi.

**19.** Teua sentensi yenye ni ya kuonyesha kiwakilishi cha nafsi.
A. Nendeni mkasome nje.
B. Tutawasili mjini mchana.
C. Walionizaini watakiona cha mtema kuni.
D. Shangazi na bintiye ni watu karimu.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

20. Jina kutokana na kitenzi <u>lia</u> ni <u>kilio</u>.
Jina kutokana na kitenzi <u>haribu</u> ni _______
A. haribika  B. uharibifu
C. harabu  D. haribia

21. Teua sentensi iliyounganishwa vyema kwa kiunganishi mwafaka.
A. Hatutakuja madhali hujatualika.
B. Waliingia darasani mbali na ruhusa.
C. Walinunuliwa vitu vingi maasam chupa ya maji, nguo na malapa.
D. Waliingia uwanjani ilhali wakanyukwa mabao mengi.

22. Kipi ni kitenzi kilichoundwa kutokana na kivumishi?
A. Kicheko-mcheshi. B. Kilimo - mkulima.
C. Mvumilivu-vumilia D. Utiifu - mtiifu.

23. Chagua usemi wa taarifa wa:
*"Tutakuja kukutembelea shuleni kwenu kesho," walisema.*
A. Walisema kwamba watakuja kunitembelea shuleni kwetu kesho.
B. Walisema kwamba wataenda kumtembelea shuleni kwao kesho.
C. Walisema kwamba wangeenda kunitembelea shuleni kwangu siku iliyofuata.
D. Walisema kwamba wangeenda kumtembelea shuleni kwao siku iliyofuata.

24. Teua wingi ulio sahihi wa sentensi hii:
*Karai lililotoboka ni hilo lako.*
A. Makarai yaliyotoboka ni hayo yenu.
B. Makarai zilizotoboka ni hizo zenu.
C. Karai zilizotoboka ni hizo zako.
D. Makarai yaliyotoboka ni hayo yako.

25. Tegua kitendawili kifuatacho:
*Bi. Kizee ana kazi daima, asubuhi na mchana.*
A. Ufagio  B. Kata
C. Ajuza  D. Chungu.

26. "Kwa" imetumikaje katika sentensi hii?
*Amefika mapema kwa Hassan.*
A. Kuonyesha kumiliki kitu fulani.
B. Kuonyesha uhusiano wa mtu na mahali.
C. Kuonyesha sababu ya kufanya jambo.
D. Kuonyesha kifaa kilichotumika.

27. Neno <u>alipoadhibiwa</u> lina silabi ngapi?
A. 10  B. 9
C. 7  D. 8

28. Ni tanakali ipi ya sauti isiyo sahihi?
A. Shilingi ilianguka majini chubwi!
B. Alipoumia alilia machozi ndo!ndo!ndo!
C. Alimwagiwa maji akalowa chepechepe!
D. Maembe yamejaa sokoni kochokocho.

29. Andika sentensi ifuatayo katika udogo:
*Nyumba zao zina milango miekundu*
A. Vijumba vyao vina vilango vyekundu.
B. Manyumba yao yana vijilango vyekundu.
C. Vijijumba vyao vina vijilango vyekundu.
D. Majumba yao yana malango mekundu.

30. Ipi si maagano?
A. Lala unono.  B. Kwaheri.
C. Buriani.  D. Chewa.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.</u>***

Hii ni karne ya ishirini na moja. Hiki ni kizazi cha kidijitali! Analogi inafyekwa na kuliwa na dijitali. Haishangazi kuwa hata vyombo vya habari ambavyo havitaki kuikumbatia dijitali, vinakufa kifo cha kipoole! Biashara zimeuliwa na dijitali. Kama vile foleni kwenye benki au kwenye mashine za ATM au hata vipochi na vifuko vya senti. Vyote hivi vimemezwa na biashara za dijitali kupitia kwenye simu.

Kizazi cha kisasa! kizazi cha karne ya ishirini na moja! Yaani watahiniwa wetu wanaofanya mtihani wa kidato cha nne sasa hivi, hawajui kitu kinachoitwa "Success cards" wao wanajua tu mitandao.

Waziri wa Elimu Prof. Magoha, anakabiliwa na ndaro za kuhakikisha kuwa ahadi yake ya kuyatangaza matokeo ya K.C.P.E hivi karibuni, wasahihishaji wamekuwa mbioni kujituma ili kuhakikisha kuwa yote yametimilika kwa wakati. Baada ya mitihani hiyo inayoendelea, wote, yaani wanafunzi waliokamilisha mtihani wa shule ya msingi na wenzangu wa kidato cha nne watajiunga na raia wengine hapa nje.

La kushtusha ni kuwa kizazi hiki kimejifunza kuwa maisha ni njia ya mkato. Kizazi ambacho kinakuzwa kwa taarifa za habari zikiwa zimetaabaliwa na visa vya wizi mbele na nyuma. Halafu wizi huo ni wa digitali. Hii ndiyo maana waziri wa Elimu ***<u>amepiga marufuku</u>*** matumizi ya simu za mkono katika maeneo ya vyumba vya mitihani.

Kizazi hiki cha kidijitali kitasaidiwa vipi? Katika siku za hivi karibuni wapo wataalamu wa kielektroniki wamejitosa uwanjani ili kuwaauni wazazi na hata walimu kujua anayoyafanya mtoto ama mwanafunzi. Wataalamu hawa wanahakikisha kuwa tunakitunza vyema kizazi chetu wakati huu wa likizo na hata baada ya likizo.

Mtandao uliofanyiwa upishi, ***ukapikwa*** na kuivishwa unawasaidia wadau mbalimbali wa elimu. Wanafunzi hawawezi kuzubaa tu majumbani. Badala tu ya kujitosa kwenye TikTok, YouTubu na kwingineko mchana kutwa, usiku kucha, sasa wanaweza kusoma kidijitali.

Mtandao huu; www.quizpops.com unafanya elimu kuwa nyepesi na sahali. Nilipoutembelea, nilishtuka na kugutuka kuwa ukiwa mzazi, mwalimu au mkurugenzi, unaweza kujua mwanao aliko na anafanya nini.

Mbali na elimu, app ya quizpops ni kama kifaa cha kuwalinda na kuwachunga watoto. Humsaidia aidha mwanafunzi kuupanua wigo wake wa kusoma kwa kutumia simu na kujikumbusha maswali muhimu sasa hivi akiwa likizoni, pasi na kukifungua kitabu.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, ni nini hakijaathirika na mfumo wa kidijitali?
A. Uwekezaji.
B. Milolongo ya benkini.
C. Biashara za vifungo.
D. Sekta ya mawasiliano.

**32.** Unadhani ni kwa nini kizazi cha sasa hakijui maana ya "success cards"?
A. Wao hujitumia wenyewe.
B. Hutumia simu zaidi kuliko kadi.
C. Hutumiwa jumbe za heri njema kupitia mtandao.
D. Mawazo yao hujikit vitabuni hivyo hawana wakati wa k.tumia kadi.

**33.** Waziri wa elimu alitoa ahadi gani?
A. Wasahihishaji watakuwa mbioni.
B. Watahiniwa wote watajiunga na raia.
C. Mtihani ungetangazwa umehelewa kuliko kawaida.
D. Watahiniwa wa shule za msingi wangejua matokeo yao kwa wakati.

**34.** Kwa mujibu wa kifungu, ni sahihi kusema
A. vijana wa sasa wamefaulu kupitia njia za mkato
B. vijana wa sasa wamejifunza kuwa hamna haja ya kulitolea jasho jambo lolote
C. vijana wa sasa wame faika sana kutokana na bidii zao.
D. serikali na walimu wamekuwa katika mstari wa mbele kuwafunza vijana njia za mkato.

**35.** Wizi wa mitihani huchangia sana na
A. wazazi B. walimu
C. mtandao D. serikali.

**36.** Kupiga marufuku ni
A. kuharamisha B. kuhalalisha
C. kuhamisha D. kuahirisha.

**37.** Nia ya wataalamu si pamoja na
A. kuwasaidia walimu kujua waliko wanafunzi
B. kuwasaidia wazazi kufahamu wafanyayo watoto
C. kuwasaidia wanafunzi kupata mafunzo bila ya kutumia vitabu.
D. kuwafaa vijana kwa kupata ajira mitandaoni baada ya masomo.

**38.** Maneno "mchana kutwa na usiku kucha" yana maana ya
A. mchana wote B. usiku wote
C. wakati wote D. asubuhi na jioni.

**39.** Mwanafunzi anaweza kutumia App ya Quizpop kwa
A. kujilinda dhidi ya marafiki waovu.
B. kupanua uelewa na kudurusu sehemu zilizomtinga.
C. kuwavizia wachache wasiopendelea kusoma.
D. kuwaongeza wengine wasiojimudu katika baadhi ya masomo.

**40.** Wadau wa elimu si pamoja na
A. walimu B. walinzi
C. wazazi D. wanafunzi.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Wanafunzi wangu wapendwa mpo? Leo katika kipindi hiki cha Kiswahili ninahiari badala ya kuendeleza na silabasi ilivyo desturi, tutajadiliana machache tu ambayo kwa mtazamo wangu yatakufaa zaidi. Sijui kama hapo ulipo umewahi kujiuliza ni kwa nini upo shuleni? Kwa nini urauka alfajiri mbichi hata kabla ya jogoo kuwika, kuja shuleni. Umewahi kujidadisi sababu zako za kuvumilia baridi kali ya asubuhi na wakati mwingine jua lichomalo utosi ba'rabara ukija shuleni ama kurejea nyumbani?

Haya yote unayafanya kwa lengo la kupata elimu. Wapo wanaofanya hivyo kwa kuwazia umuhimu wake na wapo wale wanaoshurutishwa kufanya hivyo. Yote tisa. Muhimu ni kuwa nyote mpo ili kupata elimu. Basi yategeni masikio yenu niwatongolee tongo kuhusu tija na tijara za hiki ***<u>unachokivunjia mgongo</u>***.

Elimu kwa kweli huondoa ujinga. Huku shuleni mnafundishwa maarifa na ujuzi mbalimbali kuhusu mambo tofautitofauti. Unapofunzwa utamakinika na kutambua namna ya kufanya mambo kwa kipimo. Aidha

yeyote anayepata elimu huwa mwerevu na wasiopata elimu hubaki kuwa mazuzu na mabwege ambao baadaye hujuta na kujiuma vidole.

Isitoshe elimu humvusha msomi hadi kwenye gange ya donge nono. Elimu bora humfanya mtu kuhitimu katika taaluma mbalimbali kama udaktari, uhasibu, urubani, uhandisi, ualimu, uanasheria na taaluma nyingi nyinginezo. Ama kwa hakika unapopiga darubini, utagundua kuwa wafanya kazi hawa wana pesa maridhawa za kujimudu na kuikimu familia zao. Utakula vinono, uvae nguo safi na za kisasa, uishi katika bahari ya nyumba pamoja na kuliendesha shangingi la gari. Aila yako nayo itakuwa na siha bora na pia kusomea katika shule bora. Kwani wewe huyataki maisha hayo ya kifahari?

Wanangu kukosa elimu katika enzi hizi kutakutia katika mikururo ya mikasa. Waliobobea katika elimu ndio tu watakaokuwa na satua na uwezo wa kuishi maisha bora. Kwa hivyo, tufanye takilifu kusoma ili mustakabali wetu uwe wa kupendeza. Tusijipalie makaa kwa kukosa elimu bali tufanye bidii za mchwa masomoni. Aliyeelimika hujifunza jinsi ya kuishi na wenzake kama raia mwema na hutumainiwa kuwasaidia raia wengine kuyatekeleza matilaba yao kwani kichango ni kuchangizana.

---

**41.** Kulingana na aya ya kwanza si sahihi kusema kuwa
- A. ilikuwa kawaida ya wanafunzi kusoma silabasi kila siku
- B. wanafunzi walizoea kuwahi shuleni kabla ya jogoo kuwika
- C. mwalimu alidhamiria kuwausia wanafunzi badala ya kufundisha
- D. mwalimu alikuwa na hakika kuwa wanafunzi walifahamu sababu zao kuwa shuleni.

**42.** Wanafunzi wengine
- A. hulazimishwa kuenda shuleni
- B. huenda shuleni kucheza
- C. huenda shuleni kupatana na wenzao
- D. huenda shuleni kutembea.

**43.** Kukivunjia kitu mgongo ni
- A. kukiwazia sana kitu
- B. kukifanya sana kitu
- C. kujibidiishia sana kitu
- D. kukihalalisha sana kitu.

**44.** Mtu mwenye elimu
- A. hufanya mambo mengi
- B. hufanya mambo kwa kipimo
- C. hufanya mambo haraka
- D. hufanya mambo na wengi.

**45.** Kulingana na ufahamu, taaluma zenye donge nono si pamoja na
- A. ualimu
- B. uanasheria
- C. uhandisi
- D. udereva.

**46.** <u>Uhasibu</u> ni kazi ya
- A. kuhesabu watu na pesa
- B. kuchunguza matumizi ya pesa katika shirika
- C. kutunza barua na faili katika ofisi
- D. kuweka hesabu za pesa katika kampuni au shirika.

**47.** Wenye elimu ya kutosha hufanya haya isipokuwa
- A. chakula bora na cha kutosha
- B. maisha ya kifahari na anasa
- C. mavazi bora, ghali na za kisasa
- D. kuwasomesha wanao katika shule bora nchini.

**48.** "Kwani wewe huyataki maisha ya kifahari?" Mbinu iliyotumiwa hapo huitwa
- A. balagha
- B. tashididi
- C. chuku
- D. tashihisi.

**49.** Wanafunzi wanausiwa wasome ili
- A. waishi maisha marefu
- B. wasomee shule bora nchini
- C. wavalie mavazi mazuri
- D. wabadili mustakabali wao uwe bora.

**50.** "Wanafunzi wanaombwa wasijipalie makaa". Ndiko kusema
- A. wasikalie makaa moto
- B. wasijihusishe na vikundi vya wapotovu
- C. wasijisababishie matatizo.
- D. wasijibidiishe sana masomoni.